

HALMASHAURI YA WILAYA YA KAKONKO

Simu Na. 028-2820137

Fax Na. 028-2820137

Email:ded@kakonkodc.go.tz

Tovuti :www.kakonkodc.go.tz



OFISI YA
MKURUGENZI
MTENDAJI (W)
S.L.P. 3,
KAKONKO

TAARIFA KWA UMMA NA VYOMBO VYA HABARI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko Lusubilo Mwakabibi amesaini mkataba wa Tsh.353,268,046/= na Kampuni ya Magacon Co.Ltd ya Dodoma ili kuanza kujenga ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko kwa awamu ya kwanza.

Akizungumza katika hafla ya kutia saini mkataba huo iliyofanyika katika ukumbi wa Mkutano wa Halmashauri siku ya Jumatano tarehe 14.09.2016 na kuhudhuriwa na Mhe.Mkuu wa Wilaya Col.Hosea Ndagala na Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe.Juma Maganga, Mkurugenzi amemsisitiza mkandarasi kuzingatia ujenzi wa viwango ili thamani ya fedha ionekane. Aidha ametoa wito kwa watumishi pamoja na viongozi kufanya kazi kwa moyo kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe.Juma Maganga amesisitiza ujenzi kuwa na ubora na usiotia shaka kwa manufaa ya wananchi wa Kakonko.

Mkuu wa Wilaya Col.Hosea Ndagala amemsisitiza mkandarasi kufanya kazi katika muda aliopewa badala ya kuomba kuongezewa muda na fedha zaidi.

Ujenzi wa ofisi za Halmashauri wa awamu ya kwanza utachukua kipindi cha miezi sita kwa gharama ya Tsh. 353,268,46/= kwa mujibu wa mkataba. Ujenzi utafanyika katika eneo la Kanyamfisi Wilayani Kakonko na Mkoani Kigoma. Mradi wa ujenzi wa makao makuu ya Halmashauri utakapokamilika utagharimu Tsh.1,600,000,000/= (Bilioni moja na laki sita).

Cosmas Makalla

Afisa Habari

16 Septemba, 2016